## Matukio ya Uhalifu wa Chuki na Upendeleo

**Je, Uhalifu wa Chuki ni Nini?**

Jimboni Washington, uhalifu wa chuki ni shambulio la makusudi na lenye nia mbaya, uharibifu wa mali, au tishio la shambulio au uharibifu wa mali dhidi ya mtu mwingine kutokana na jamii yake, rangi, dini, asili, kabila, taifa, jinsia, mwelekeo wake wa kijinsia, jinsi mtu huyo anavyojisikia au kujitambulisha kijinsia, au ulemavu wa akili, mwili, au hisia zake.

Uhalifu wa chuki ni kosa la jinai lenye adhabu kali jijini Washington, lenye kifungo cha hadi miaka mitano gerezani na/au faini ya hadi dola 100,000. Mwathirika wa uhalifu wa chuki pia anaweza kufungua kesi ya madai dhidi ya mhalifu kudai fidia halisi, fidia ya adhabu hadi dola 100,000, na gharama za mawakili pamoja na gharama nyingine zinazotokana na kufungua kesi hiyo (Revised Code of Washington (RCW, Kanuni Zilizorekebishwa za Jimbo la Washington) 9A.36.080).

**Je, Tukio la Upendeleo ni nini?**

Katika Jimbo la Washington, tukio la upendeleo ni tendo au kauli ya uhasama inayoonyesha chuki dhidi ya mtu mwingine, **kutokana na jamii yake, rangi yake halisi au inayodhaniwa, asili ya taifa, dini, imani, ukoo, uraia au hali ya uhamiaji, jinsia, hadhi ya kuwa mwanajeshi au mstaafu aliyeheshimiwa, mwelekeo wa kijinsia, au uwepo wa ulemavu wa kihisia, kiakili, au kimwili, au matumizi ya mbwa msaidizi au mnyama wa usaidizi kwa mtu mwenye ulemavu** (RCW 43.10.305(5)(a)). Orodha ya sifa hizi inajumuisha sifa zilizotajwa katika sheria ya uhalifu wa chuki ya Jimbo la Washington pamoja na makundi yanayolindwa chini ya Washington Law Against Discrimination (Sheria ya Washington Dhidi ya Ubaguzi) (RCW 49.60.030(1)).

"Tendo au kauli ya uhasama inamaanisha kutoa maoni ya chuki au upendeleo kwa njia isiyo ya heshima, isiyo rafiki, au ya fujo. **Tukio la upendeleo ni tukio ambalo halifikiki kiwango cha kuwa kosa la jinai au tendo la uhalifu.** Mifano ya matukio ya upendeleo ni pamoja na lakini si tu:

- Kutumia lugha ya matusi dhidi ya mtu mwingine kutokana na sifa zake zinazodhaniwa au kuwa mmoja wa washirika wa kundi linalolindwa.
- Kuchora au kuunda picha za kibaguzi au za matusi kulingana na sifa zinazodhaniwa za mtu huyo husika au uanachame wake katika kundi linalolindwa.
- Kumdhihaki mtu mwenye ulemavu au kudhalilisha mila na desturi za mtu mwingine.

RASIMU

**Nambari ya Simu ya Matukio ya Uhalifu wa Chuki na Upendeleo**

Washington Attorney General's Office (AGO, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Washington) iliagizwa kuanzisha Hate Crimes & Bias Incidents Hotline (Nambari ya Simu ya Matukio ya Uhalifu wa Chuki na Upendeleo) chini ya Senate Bill (SB, Muswada wa Seneti) 5427 (2024), uliopitishwa na bunge mwaka 2024 na kuwekewa kanuni katika RCW 43.10.305. Nambari hii ya simu lazima iwapatie wanaopiga simu taarifa na marejeleo ya huduma za karibu, zinazomlenga mhanga, zinazozingatia tamaduni, na zinazotambua athari za mshtuko, na kadri inavyowezekana, ziweze kupatikana kwa lugha mbalimbali. Nambari ya Simu itapatikana katika kaunti za Clark, King, na Spokane kuanzia Julai 1, 2025, na itapatikana katika ngazi ya jimbo zima kuanzia Januari 1, 2027. **Nambari ya Simu si ya dharura, na wapigaji simu wataelekezwa kupiga 911 ikiwa wanaripoti tukio la dharura.**

**Kila mtu ambaye amekuwa mhanga wa chuki au upendeleo anaweza kupiga Nambari hiyo ya Simu kuripoti tukio na kupokea taarifa kuhusu huduma, bila kujali hali yake ya uhamiaji. Huduma za ukalimani zitapatikana.** Watoa huduma ambao Nambari hiyo ya Simu itawaunganisha na wapiga simu watatoa huduma mbalimbali, zikiwemo za afya ya mwili na akili; msaada wa kisheria; msaada unaozingatia tamaduni; na utetezi wa wahanga.

**Taarifa binafsi zinazotolewa kwenye Nambari ya Simu zinahifadhiwa kwa usiri na hazitawekwa hadharani.** Taarifa hizi zinajumuisha jina, jina la awali la kisheria, jina la utani, jina la mama kabla ya kuolewa, tarehe au mahali pa kuzaliwa, makazi, anwani ya barua, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, nambari ya mfuko wa hifadhi ya jamii, nambari ya leseni ya udereva, nambari ya akaunti ya benki, na taarifa nyinginezo za utambulisho (RCW 43.10.305(5)(g)).

Kulingana na sheria, huduma ya Nambari ya Simu lazima iulize kama anayepiga simu amewahi kuripoti kwa mamlaka za sheria na ikiwa angependa kufanya hivyo. **Huduma ya Nambari ya Simu itahusisha vyombo vya sheria ikiwa tu mpiga simu amekubali** na itashiriki tu taarifa za utambulisho ambazo mpiga simu ametaka zishirikiwe. Mamlaka za sheria zinahitajika kutoa taarifa za mawasiliano ya Nambari hiyo ya Simu kwa mtu yeyote anayeripoti tukio la chuki au upendeleo.

RASIMU